# Jarida La MELI

MARINE SERVICES COMPANY LTD — KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

**TOLEO LA 3 JANUARI - MACHI 2021**




ZIJUE HATUA MUHIMU ZA KUJIOKOA MAJINI.

UK. 2



MAKALA MAALUM YA MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

UK. 8



MSCL YAFANYA UTAFITI WA MASOKO GANA NA GODZIBA

UK. 11



# KAMATI YA BUNGE YAMPONGEZA RAIS SAMIA UJENZI WA MV MWANZA

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mh. Seleman Kakoso akiongea na waandishi wa Habari muda mfupi baada ya kamati hiyo kukagua mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza.

*Na Edmond Rutajama*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi wa ujenzi meli ya MV Mwanza ili kurahisisha usafiri na usafirishaji katika mikoa inayozunguka Ziwa Victoria na nchi Jirani.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo jijini Mwanza, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mh. Seleman Kakoso amesema kuwa Serikali ya awamu ya sita imeendelea kutoa fedha ili kuendeleza mradi huo kwa dhamira ya kukuza pato la mikoa ya kanda ya ziwa na Serikali kwa jumla baada ya mradi kukamilika.

"Naipongeza sana Serikali hasa Mhe Rais sababu taarifa tuliyopewa hapa ni kuwa mkandarasi ameshalipwa 'Certificate' (vyeti) zote alizowasilisha kilichobaki ni sisi kama watanzania kujiweka tayari kwa meli hiyo kukamilika," alisema Mhe. Kakoso.


Mhe. Kakoso ameeleza umuhimu wa kuzingatia mahitaji ya rasilimali watu hasa kwenye taasisi zenye miradi mikubwa na kusisitiza kuwa uwepo wa watumishi wa kutosha kwenye kada muhimu kama uhandisi na manunuzi kutaongeza tija na uzoefu kuanzia mwanzo wa miradi mpaka uendeshaji wa miradi inapokamilika.

Aidha Mhe. Kakoso ameitaka Wizara kusimamia Taasisi zinazofanya kazi kwa karibu ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Huduma Meli (MSCL) na Shirika la Reli ya Tanzania (TRC) ili kuhakikisha mipango ya taasisi hizo inakwenda pamoja ili kuepuka kupishana kwenye utekelezaji wa miradi.

Naye Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, amemuhakikishia Mwenyekit na wajumbe wa Kamati hiyo kuwa tayari Serikali imeshatoa maelekezo kwa taasisi hizo kushirikiana ili miradi itakapokamilika kusiwe na visingizio kwenye uendeshaji.

Mhe. Mwakibete ameeleza kuwa pamoja na juhudi mbalimbali zinazoendelea tayari MSCL, TPA na TRC zimeshatiliana saini makubaliano maalum ya kusafirisha mizigo ikiwa ni moja ya jitihada ya ushirikiano.

# MV MWANZA NA MV UMOJA MKOMBOZI WA USAFIRI ZIWA VICTORIA



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) Mhe. Atupele Mwakibete (wa mbele) akiteremka kutoka kukagua mradi wa MV Mwanza unaoendelea kutekelezwa katika bandari ya Mwanza Kusini.*

*Na Fatina Msangi*

Imeelezwa kuwa kukamilika kwa ujenzi wa meli ya MV Mwanza na Ukarabati wa meli ya MV Umoja kutarahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji kwa mikoa inayozunguka Mkoa wa Mwanza pamoja na nchi Jirani zinazotumia Ziwa Victoria.

Kauli hiyo imetolewa jijini Mwanza na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete mara baada ya kukagua maendeleo ya ukarabati na ujenzi wa meli hizo kusema Serikali itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha miradi yote ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

"Nipende kuwahakikishia kuwa kukamilika kwa ujenzi wa meli ya MV Mwanza kutatochea sana uchumi na kuongeza pato kwa mikoa inayozunguka ziwa lakini pia kukamilika kwa ukarabati wa MV Umoja kutarahisisha sana usafiri wa abiria na mizigo", amefafanua Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete ameitaka MSCL kuhakikisha inawasimamia kwa karibu Wakandarasi wote wawili wanaotekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati ili wakamilishe miradi hiyo kwa kuzingatia thamani ya fedha lakini kuongeza ujuzi kwa wataalaam wa ndani.

Aidha, Naibu Waziri Mwakibete ameihakikishia MSCL kuwa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ikiwemo upungufu wa watumishi wa fani za uhandisi kuwa litashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi ili kufanya taasisi hiyo iweze kuwa imara kiutendaji.

Kwa upande wake, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL, Philemoni Bagambilana, amemuhakikishia Naibu Waziri huyo kuwa taasisi imejipanga na inasimamia kwa karibu miradi hiyo ili kuleta matokeo ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika ukanda huo.

Bagambilana ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza kwenye taasisi hiyo na kusema moja ya matokeo ya uwekezaji kwenye ukarabati wa meli hasa za MV Victoria na MV Butiama ni kuongezeka kwa mapato kutoka bilioni takribani 1 kwa mwaka 2019 hadi kufikia bilioni takribani 4.5 mwaka 2021.

Mradi wa Ujenzi wa Meli ya MV Mwanza unatekelezwa na Kampuni ya Gas Entec Company Limited na Kampuni ya KANGNAM Corporation kwa kushirikiana na SUMA JKT kwa gharama ya shilingi bilioni 96.9 na ukarabati wa Meli ya MV Umoja unatekelezwa na SM Solution Co ltd ya nchini Korea na unagharimu kiasi cha shilingi bilioni 19.



*Baadhi ya Wajumbe wa baraza la Wafanyakazi MSCL wakisikiliza kwa makini mawasilisho mbalimbali wakati wa kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi mdogo wa semina uliopo katika eneo la bandari ya Mwanza Kusini. (Picha na Edmond Rutajama)*




# ZIJUE

## SEHEMU TANO ZA KOTI LA UOKOAJI NA HATUA MUHIMU KUJIOKOA MAJINI

*Mfanyakazi wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu Nahonge Deus akionesha namna ya kutumia koti la kujiokolea (Life Jacket). (Picha na Edmond Rutajama)*

***Na Fatina Msangi***

INAPOTOKEA ajali ya meli, ikatoa mwanya wakuvaa koti la uokoaji (life jacket), baada ya kuvaliwa ipasavyo na kabla ya kujirusha kwenye maji,abiria atumie mkono wa kulia kulishikilia (koti) vizuri ubavuni kushoto, huku mkono wa kushoto ukiziba pua na mdomo, ndipo ajitupe kwenye maji.

Kushikilia koti kutazuia mawimbi mazito ya maji wakati wa kujirusha yasilisukume likavuka na kumuweka abiria katika hatari ya kifo.

Na kuziba uso ni kuzuia maji yasiingie puani na mdomoni wakati wa kujirusha kwenye maji, hali inayoweza kusababisha madhara vilevile kwa abiria.

"Uso unazibwa kwa muda mfupi kwani haitachukua hata dakika abiria kuibuka baada ya kujirusha kwenye maji.

"Na kwa mwelekeo wowote ule alioingia nao kwenye maji,baada ya kuibuka lazima sehemu za koti zilizotuna mbele zitamgeuza alale chali na kuelea kwa starehe," anasema Baharia wa Meli ya 'MV Victoria Hapa Kazi Tu", Elias Kapinga.

Anasema kwa lugha ya kibaharia meli inapopata matatizo ni "dharura" na si ajali na kwamba kawaida dharura nyingi za meli humpa abiria nafasi ya kuvaa koti, labda tu kama meli imepinduka.

Kutokana na fursa hiyo ya kuvaa koti, Kapinga anashauri pia mwenye uwezo wa kujirusha kwenye maji na viatu afanye hivyo au abaki na soksi ili kuepuka kushambuliwa na samaki sehemu za nyayo.

Anasema mtu akiwa kwenyemaji nyayo humeremeta na kuwavutia samaki kuzishambulia.

"Wanazishambulia kwa mtindo wa kudonoa kidogo kidogo, akichelewa kuokolewa atapata majeraha makubwa," anasema.

Anaelimisha zaidi kwamba ikitokea abiria wamejirusha kwenye maji bila kufunika nyayo na wakakutana kikundi (kwenye maji), basi watengeneze umbo la duara kwa kushikana mikono na kila mtu agusanishe nyayo na aliyetazamana naye ili kuzuia mmeremeto wa nyayo kuepuka kushambuliwa na samaki.

"Wakati huo huo mzamaji atumie vifaa vilivyopo kwenye koti kuita vyombo vya uokoaji. Hata hivyo, abiria wasijirushe kwenye maji kabla ya nahodha mkuu kuwatangazia kufanya hivyo kwani upo uwezekano wa waokoaji kuwakuta kwenye meli yao, kama haizami," anasema.

Anasema kusubiri maelekezo ni muhimu kwani hata boti za uokoaji zilizomo ndani ya meli iliyopata dharura zinaweza kufanya uokoaji, kama meli haikupinduka.

Kwa mujibu wa Kapinga,koti lina sehemu kuu tano ikiwemo viakisi mwanga (reflector) ambavyo husaidia mtu kuonekana kwa waokoaji.

Sehemu nyingine ni filimbi inayokua ikining'inia mbele kwenye koti ambayo mzamaji ataipuliza kuita waokoaji.

Kapinga anasema filimbi ni rahisi kuomba msaada kwani sauti yake inasafiri masafa marefu kuliko ya binadamu.

Inaelezwa kwamba koti pia lina kamba mbili mbele, ndefu na fupi ambapo kazi ya kamba ndefu ni pale ambapo chombo cha uokoaji, hasa boti kitakua kimemfikia mlengwa, atarusha Kamba hiyo na itafungwa sehemu yoyote ya chombo na kumvuta.

Chombo kitaacha nafasi ya hatua kadhaa ambapo kamba hiyo ndefu itaweza kukifikia kwani kikimkaribia sana mzamaji, mawimbi yanaweza kukifanya kimsukume mbali zaidi.

"Na kamba fupi imepachikwa karibu na bega ambayo hutumika kwa uokoaji wa vyombo vya angani, hasa helikopta,"anasema Kapinga na kufafanua

*Inaendelea uk. wa 10*

# Nini kitatokea baada ya meli ya MV Mwanza kushushwa ziwani

*Na. Abdulrahman Salim*

Wahandisi wa meli wanaamini kuwa elimu ya uundwaji wa meli ni wa karne nyingi sana na ulianza kabla ya gari, ndege, pikipiki na hata baiskeli. Historia katika vitabu vya dini inatuambia kuwa uundwaji wa meli ulianza kipindi cha Nabii Nuhu, ambaye alijenga jahazi kubwa lililoweza kubeba viumbe wa kila aina.

Karne ya 21 imeitwa karne ya sayansi na teknolojia kwakuwa mengi yameboreshwa kuliko hata ilivyokuwa miaka 100.

Meli ya MV Mwanza ni miongoni mwa meli za kisasa na kubwa kuwahi kutokea katika ukanda wa Ziwa Victoria. Meli hii inajengwa kukamilisha ahadi ya miaka 26 iliyopita baada ya meli ya MV Bukoba kuzama na serikali kuahidi kujenga meli itakayokuwa mbadala wa MV Bukoba.

MV Mwanza inatarajiwa kushushwa katika maji mwezi Septemba, 2022 kwaajili ya uchunguzi wa maeneo hatarishi saa 72 kabla ya meli hiyo kuendelea na taratibu za kuanza kutoa huduma kwa wakazi wa kanda ya ziwa pamoja na nchi jirani za Uganda na Kenya.

Vitus Mapunda ni Meneja mradi wa meli ya MV Mwanza anaeleza juu ya maeneo manne hatarishi ambayo yanaweza kusababisha meli kurudi kwenye chelezo baada tu ya meli hiyo kushushwa.

"Eneo la kwanza linaloweza kuingiza maji ni eneo la Shafti za kuisukuma meli, ambalo ni kama matairi ya meli, inawezekana kwa makosa ya kibinadamu maji yanaweza kuingia kupitia kwenye sehemu hiyo, hilo litajulikana endapo meli itashushwa kwenye maji na kuhakikisha kuwa maji ya ziwa hayawezi kupita kwenye eneo hilo, kwahiyo uhakika wa mwisho ni mpaka meli inaposhushwa kwenye maji."

Mapunda alisema kuwa eneo la pili ni la mbele ya meli ambapo kuna kifaa kinaitwa bow thruster kwaajili ya kumwezesha nahodha kukata kona kwa urahisi, na kuongeza kuwa kifaa hicho kinaongeza uwezo wa meli kuwa na uhuru wa kwenda kulia (star board) na kushoto (port side) badala ya kuwa na uhuru wa kwenda mbele na kurudi nyuma.

"Katika lugha ya meli wanaita kwenda star board na port side hawakubali maneno ya kusema kulia na kushoto kwasababu wanasema kulia na kushoto kunategemea wewe umekaa wapi na unaangalia wapi, lakini ukisema star board na port side vyovyote itakavyokuwa star board itabaki kuwa star board na port side itabaki hivyo na hiyo ndivyo inavyotumika hata kwenye ndege," alifafanua.

Halikadhalika, eneo la tatu hatarishi ni eneo linaloingiza maji ndani ya meli kwaajili ya kupoza mitambo ya meli. Maji hayo huzunguka kwenye injini na kutengeneza joto na kupita kwenye kifaa kinachoitwa heat exchanger. Kifaa hicho kina upande wa ndani wenye maji ya moto yanayotoka kwenye injini na upande wa nje kuna eneo linaloruhusu maji kutoka nje kuingia na kupoza maji yanayotoka kwenye injini kwa kuizunguka heat exchanger na kutoka nje.

"Kuna maji ambayo yanaingia na kutoka na yanazunguka muda wote wa safari au muda wote unapowasha injini, na maji hayo huonekana pembezoni mwa meli yakimwagika, yale maji unayoyaona pembeni yanamwagika kwenye meli ni maji ambayo yametoka ziwani au baharini yakaingia kwenye meli yakapita kwenye kifaa kinachoitwa heat exchanger yakapooza maji ambayo yametoka kwenye injini na kumwagwa tena nje, uhakika wake kama yanaingia bila ya udhibiti yatafanyika eneo hilo."

Lakini eneo la nne ni la uchomeleaji, chuma na chuma kimeunganishwa na macho ya mwandamu au makosa ya mwanadamu yanaweza yakapelekea maji yakawa yanaingia kwenye miunganiko hiyo kutokana na kushindwa kufanikisha zoezi hilo kwa asilimia mia moja, maeneo hayo yatahakikiwa wakati meli itakapokaguliwa ndani ya saa 72, na kuonesha kama kuna udhaifu wowote unaohitaji marekebisho,

"Kuna udhaifu ambao tutalazimika hii meli tuipandishe tena na tukilazimika hakutakuwa na jinsi ya kufanya bali tutairudisha kwenye chelezo, lakini kuna udhaifu mwingine wa maji kuingia siyo kwasababu kuna makosa ya kihandisi bali mtendaji amesahau kufunga valve, kwahiyo tukijihakikishia kuwa hayo maji yanapita kwenye hiyo valve litakuwa ni suala la kufunga lakini yakipita kwenye sehemu ambayo inahitaji uchomeleaji na hatuwezi kuchomelea katika maji kwasababu hatuna vifaa hivyo, basi italazimika meli tuirudishe kwenye chelezo na kufanyiwa kazi pale mahala ambapo pana udhaifu," alieleza.

Mradi wa Ujenzi wa Meli ya MV Mwanza unatekelezwa na Kampuni ya Gas Entec Company Limited na Kampuni ya KANGNAM Corporation kwa kushirikiana na SUMA JKT kwa gharama ya shilingi bilioni 96.9



*Muonekano wa Meli ya MV Mwanza kwa upande wa kushoto (port side). (Picha na Abdulrahman Salim)*




Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wakiongozwa na Meneja Tawi la Mwanza Nahodha Bembele Ng'wita walipohudhuria katika mazishi ya Baba Mzazi wa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL, Philemon Bagambilana katika Kijiji cha Kyaka, Wilayani Karagwe, Mkoani Kagera mapema mwezi wa February, 2022.

# HABARI PICHA



Afisa Masoko Mkuu, ndugu Eugenia Punjila akishiriki kutoa zawadi kwa wateja wa meli ya New Butiama hapa kazi tu wakati wa sherehe za Mwaka mpya 2022. (Picha na Abdulrahman Salim)



Picha ya pamoja iliyowahusisha wadau wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) katika mkutano wa maandalizi ya Mpango wa Biashara wa Kampuni uliofanyika Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Anselm Namala (wa pili toka kushoto waliokaa). (Picha na Deo Mganga)



Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) walioshiriki katika maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani tarehe 08.03.2022 (Picha na Edmond Rutajama)

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ikiwasilishwa na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Bwana Philemon Bagambilana (kulia) alipoungana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Reli Uganda (URC), Shirika la Reli Tanzania (TRC) pamoja na Shirika la Uwezeshaji wa Usafiri wa Ushoroba wa Kati (CCTTFA) kusaini Makubaliano ya Kodi ya Huduma (Service Levy Agreement – SLA) pamoja na Roofing Mills na Mratbu Nunu Logistics kusafirisha shehena kutoka Dar es Salaam kwenda Kampala nchini Uganda. (Picha na Anselm Namala)



# Kamati ya Bunge ya miundombinu yaitahadharisha MSCL



*Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge pamoja na watumishi wa MSCL wakiwa katika eneo linalotumika kuunganishia meli inayobeba mabehewa na reli ya nchi kavu (Link Span) katika bandari ya Mwanza Kusini. (Picha na Abdulrahman Salim)*

*Na Abdulrahman Salim*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imewataka watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuwa wazalendo na kutumia fursa waliyopewa na Serikali ya kuifufua Kampuni hiyo na kutengeneza mazingira ya kuishawishi Serikali iwaamini zaidi.

Akizungumza wakati wa majumuisho ya ziara baada ya kamati hiyo kukagua na kutemebelea ya miradi ya ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza pamoja na Ukarabati wa meli ya MV Umoja inayotekelezwa na Serikali kupitia MSCL Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Seleman Kakoso alisema kuwa historia inaonesha kuwa huko nyuma walioiua MSCL walikuwa ni wafanyakazi.

"Ninyi wafanyakazi ndio wenye dhamana lakini mkiiua ile miundombinu inayojengwa na serikali, waathirika wakubwa ni ninyi wafanyakazi. Mlishuhudia miezi 27 mlikuwa hamlipwi mishahara ni kwasababu serikali ilibaini MSCL ilikuwa ni chombo kama kilichofanywa kama cha watu binafsi. Zilikuwa tiketi zinakatwa, za kampuni zinakuwa chache za watu binafsi zinakuwa nyingi, haya yasije yakajirudia tena." Alisisitiza

Aidha, Mhe. Kakoso alikitaka kitengo cha masoko kuonesha ubunifu na kuzidisha jitihada za kutafuta masoko kwenye maeneo husika na kutahadharisha kuwa miundombinu inajengwa lakini mifumo ya masoko bado iko chini na hivyo kuiomba Wizara kuisaidia MSCL ili kufanikisha zoezi hilo.

"Hii miundombinu tunayoijenga kama haitakuwa na mifumo ya masoko tunachokifanya ni sawa na hakuna, nendeni nchi jirani ya DRC mkatengeneze mifumo ya kuwashirikisha ili waweze kutumia huduma zile tunazokusudia. Lakini nendeni Kenya na Uganda kama mlivyosema mna maafikiano ambayo mmeweka sasa ili tuweze kwenda vizuri lazima (wizara) muwabebe hawa kwa kuwashawishi wafanyabiashara watumie miundombinu ya kwetu, hili tukiwaachia hawa peke yao hawataweza kusimama," Alisema.

Vile vile, Mhe. Kakoso alisema kuwa Kamati imebaini ufa uliyopo kati ya taasisi ambazo zinaingiliana na kubainisha kuwa Mamlaka ya Bandari (TPA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na MSCL hawana muunganiko thabiti na hivyo kuitaka Wizara iweze kuwaunganisha ili miradi inapojengwa wajipange kwa utekelezaji.

"Mamlaka ya Bandari kwa mkoa wa Mwanza miundombinu yake si mizuri na wakati huo huo tuna uwekezaji mkubwa sana ambao unahitaji sana kuwa na masihirikiano na nchi za jirani za Kenya na Uganda. Naomba ile miundombinu ambayo ina muingiliano kati ya MSCL, Shirika la Reli na Mamlaka ya Bandari isimamieni ikae vizuri ili uwekezaji uendane na uhalisia wa kile kilichowekezwa na serikali." Alifafanua.

Hata hivyo, Mhe Kakoso aliiomba Serikali kuendelea kuwasimamia wakandarasi ili waweze kukamilisha miradi kwa muda uliopangwa.

"serikali kumekuwa na lugha ambazo kila mara mradi unapokwama kisingizio kikubwa sana ni "Covid". Sasa tukiwasikiliza hawa wakandarasi kwa haya majibu ya "Covid" ipo miradi mingi ambayo itasimama hapa nchini kwasababu wanakuja kuomba kazi na Covid ikiwepo lakini machafuko ya dunia hii sio "Covid" tu kuna vita huko ya Ukraine na Urusi, tatizo la Ukraine limeanza kuathiri shughuli zingine naomba sana Mhe. Naibu Waziri kashirikianeni kama wizara muhakikishe mnawasimamia wamalize hii miradi kwa wakati," Alielezea.

Katika hatua nyingine Mhe. Kakoso ameishauri Serikali kuwabeba na kuwaendeleza vijana wa kitanzania walioshiriki kwenye mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza ili kuja kuisaidia Serikali katika Miradi mingine ambayo imeanzishwa na inayotegemewa kuanzishwa.



# MAKALA MAALUM



## MWAKA MMOJA WA UONGOZI WA SERIKALI AWAMU YA SITA CHINI YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN

## SSH

# MIRADI YA MELI YATEKELEZWA KWA KASI NDANI YA MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

*Na Abdulrahman Salim*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitasahau siku ya tarehe 19.03.2021 ambapo historia mpya ya nchi iliandikwa baada ya kumpata Rais Mwanamke anayeongoza Serikali ya Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyerithi kiti cha urais baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kilichotokea tarehe 17.03.2021.

Sasa ni mwaka mmoja tangu serikali ya awamu ya sita kushika hatamu katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi lenye kubebwa na kauli mbiu ya "Kazi iendelee" iliyotolewa na Mhe. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake ya kwanza akiwa katika kiti hicho cha urais.

Katika kipindi hiki maendeleo mengi yamefanyika katika sekta mbalimbali nchini ikiwemo sekta ya Uchukuzi, chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo inaisimamia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), inayomiliki boti moja na meli 14 za serikali zilizopo katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Katika kuendelea kuboresha huduma za usafiri kwa njia ya maji na kuboresha usafiri na usafirishaji katika ushoroba wa kati, serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 125.1 katika mradi wa ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu katika Ziwa Victoria, na miradi miwili ya ukarabati wa meli mbili za MV Umoja inayobeba mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria pamoja na MT Sangara kwa ajili ya kubeba mafuta katika Ziwa Tanganyika.

Mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza unathamani ya shilingi bilioni 96.9 na unatekelezwa na Mkandarasi GAS Entec Co. Ltd kutoka Korea Kusini, meli hii itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ikiwemo magari makubwa matatu na magari madogo 20.

Wakati akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa mradi wa MV Mwanza Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL Philemon Bagambilana alisema kuwa mradi huo umefikia asilimia 64 na unategemewa kukamilika mwezi Septemba, 2022 huku ukiwa umetengeneza ajira 150, kati yao 12 wakiwa ni wanawake.

"Mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 lakini chini ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali imetenga shilingi 20,295,147,767.00 ambapo hadi sasa tumeshapokea shilingi 7,901,382,155.78 ili kutekeleza mradi huo," Alieleza.



*Meli ya MV Umoja ikiwa chelezoni kwaajili ya ukarabati*

Aidha, mara tu mradi wa ukarabati wa meli ya MV Umoja utakapomalizika, meli hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba mabehewa 21 ambayo ni sawa na tani 1,200 badala ya uwezo wa sasa wa kubeba mabehewa 19, hali hii itaongeza tija katika usafirishaji wa mabehewa katika Ziwa Victoria.

"Mradi wa ukarabati mkubwa wa meli ya MV Umoja unatekelezwa na mkandarasi SM Solution kutoka nchini Korea Kusini na ulianza utekelezwaji tarehe 25.11.2021, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 serikali imetenga fedha zote zitakazokamilisha ukarabati wa meli hii ambayo ni shilingi 19,811,446,192.00, na mpaka mwezi Februari, 2022 serikali imeshalipa shilingi 2,919,726,948.96 na mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 15, na hadi sasa ukarabati huo umefikia asilimia 23," Bagambilana alifafanua.

Kwa upande wa Ziwa Tanganyika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 serikali ya awamu ya sita imetenga kiasi cha shilingi 8,484,875,397.00 katika mradi wa ukarabati wa meli ya MT Sangara unaotekelezwa na Mkandarasi KTMI Co. Ltd, meli hii ina uwezo wa kubeba mafuta lita 410,000 sawa na tani 350 na inatoa huduma katika Ziwa Tanganyika.

Serikali imeshatoa kiasi cha shilingi 1,272,731,309.55 katika utekelezaji wa mradi huu ambao umeshafikia asilimia 25 na unatakiwa kukamilika ndani ya miezi 12.

"Halikadhalika, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja wa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tunatarajia kuanza safari mpya za visiwani, visiwa vya Gana na Godziba kutokea mwalo wa Kirumba kwa kutumia meli yetu ya MV Clarias, hii ni katika kuendelea kutoa huduma za usafiri majini, safari hizi tunazianza ndani ya mwaka huu mmoja wa uongozi wa serikali ya awamu ya sita," Bagambilana alisema.

Pia, Meli ya MV Wimbi yenye uwezo wa kubeba tani 120 za mizigo itaambatana na meli ya MV Clarias katika safari hizo za visiwa vya Gana na Godziba ili kuimarisha usafirishaji wa mizigo kwa njia ya maji kwa wananchi wanaoishi katika visiwa hivyo.

Hadi mwezi Machi 2022, MSCL ina meli nne zinazofanya kazi ikiwemo meli ya New Butiama yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo inayosafiri kutoka Mwanza kuelekea Nansio, Wilayani Ukerewe, meli ya New Victoria yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo inayosafiri kutoka Mwanza kuelekea Bukoba, Mkoani Kagera, pamoja na meli za MV Clarias yenye uwezo wa kubeba abiria 216 na tani 10 za mizigo pamoja na meli ya ML Wimbi yenye uwezo wa kubeba tani 120 za mizigo zitakazoanza kufanya safari za kutoka Mwanza kuelekea visiwa vya Gan ana Godziba.

MSCL ni Kampuni ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambapo kabla ya kusajiliwa rasmi mwaka 1997 ilikuwa ni kitengo cha usafiri kwa njia ya maji katika Shirika la Reli (TRC) nchini.

# ZIJUE SEHEMU TANO ZA KOTI LA UOKOAJI NA HATUA MUHIMU KUJIOKOA MAJINI

*Inatoka ukurasa wa 3*

kwamba helikopta itamkaribia mzamaji na kuingiza kamba hiyo fupi katika sehemu maalumu kisha kumvuta juu.
Katika koti la uokoaji ipo pia taa inayoning'inia mbele ambayo baada ya abiria kujirusha kwenye maji itajiwasha yenyewe na kuwaonesha waokoaji mtu alipo.
Mzamaji anaweza pia kuiwasha taa hiyo kwa

**"Uso unazibwa kwa muda mfupi kwani haitachukua hata dakika abiria kuibuka baada ya kujirusha kwenye maji**

mkono wake, baada ya kulala chali endapo ataona inachelewa kujiwasha yenyewe. Upo uzi ambao mzamaji atauvuta kwenda chini ili iwake.
Sehemu nyingine muhimu kwenye koti la uokoaji ni jina la meli iliyopata dharura ambalo limeandikwa mgongoni ili endapo itatokea mzamaji akasukumwa na upepo kwenda sehemu isiyostahili, ikiwemo nchi nyingine basi iwe rahisi kumtambua na kumpeleka kunakostahili.
Anashauri pia kwamba wakati wa kuvaa koti abiria mwenye simu anaweza kuiviringisha vizuri kwenye mfuko wa plastiki, ajirushenayo kwenye maji ili imsaidie kwa mawasiliano atakapokua amelala chali.

Ikitokea dharura anawashauri abiria kuvaa koti kwa usahihi, kuhakikisha vishikizo vyote viwili vya mikanda vilivyopo chini na juu upande wa mbele (wa koti) vimebana ipasavyo ili wawe salama muda wote wa kusubiri kuokolewa.

"Akishalala chali hata kitabu anaweza kusoma kwani koti linamlinda hawezi kugeuza mkao.Na ndipo hata simu ataweza kupiga na kuokolewa akiwa salama," anasisitiza.
Endapo meli imepata dharura isiyotoa mwanya wa kuvaa koti, mfano kupinduka,basi abiria ashike chochote kitakachokua mbele yake, iwe ubao, tairi la gari au mkungu wa ndizi ambayo kwa kawaida huwa havizami.
Katika meli ya New Victoria Hapa Kazi Tu makoti hayo huwekwa katika kila chumba na kila kitanda na kwenye masanduku maalumu yaliyopo katika eneo la boti za uokoaji na katika meli ya New Butiama hapa Kazi tu makoti hayo huwekwa katika masanduku maalum yaliyopo eneo la kuingia ndani ya meli.



*Mfanyakazi wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu Nahonge Deus akionesha namna ya kutumia koti la kujiokolea (Life Jacket). (Picha na Edmond Rutajama*


## SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

### BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI - PHILEMON BAGAMBILANA
MHARIRI - ABDULRAHMAN SALIM

WAJUMBE

ANSELM NAMALA
BARAKA BIGAMBO
MHANDISI ABEL GWANAFYO
NAHODHA BEMBELE NG'WITA


TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

# MSCL YAFANYA UTAFITI WA MASOKO VISIWA VYA GANA NA GODZIBA

*Na Fatina Msangi.*

Hakika safari ni hatua, baada ya Meli ya MV Clarias kufanyiwa maboresho na kuwa tayari kwaajili ya kuwahudumia wananchi. Timu ya utafiti ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilifika katika visiwa vya Gana na Godziba na uongozi wa visiwa hivyo ili kuwawasilishia ujumbe wa maadalizi ya meli za MV Clarias na ML Wimbi kufanya safari za kutoka Mwanza kwenda Godziba kupitia kisiwa cha Gana.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Anselm Namala ndiye aliyeongoza timu hiyo akiwa pamoja na pamoja na Meneja wa MSCL Tawi la Mwanza, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Mhandisi wa Usimamizi wa meli (maintenance engineer), Mhasibu, pamoja na mabaharia wanaohudumu katika meli hiyo wakiongozwa na Nahodha wa meli ya MV Clarias.

Timu hiyo ilifanikiwa kuongea na wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara pamoja na wananchi wa visiwa juu ya ratiba ya kuanza safari za hizo za visiwani.



*Mkuu wa kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Anselm Namala akiongea kwenye mkutano wa hadhara katika Kisiwa cha Godziba. (Picha na Abdulrahman Salim)*


*Timu ya Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli walioshirki katika utafiti wa kutafuta masoko katika visiwa vya Gan ana Godziba. (Picha na Abdulrahman Salim)*

**SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESABIWA**




**KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL)**

BANDARI YA MWANZA KASKAZINI, JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA, Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz Tovuti: www.mscl.co.tz

Kampuni ya Huduma za Meli | MSCLtz | mscltz | Meli TV

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI NCHINI